

# Uzima

**Toleo la 09**

hello@dignityonline.org.uk

+447340 573 937

## Moto Huenea!

Mwali mdogo, hivyo ndivyo huanza. Hakuna mtu aliyejua ingeweza kuongezeka pakubwa hivyo. Grace alikuwa ameagizwa kufyeka kandokando ya moto, iwapo tu moto ungeenea.

Grace hakufanya kazi nzuri hata hivyo. Unyasi mdogo ulilala na kuegemea sehemu iliyofyeka kuelekea motoni. Iligharimu tu upepo kidogo na ghafla mwali uliwaka na huo unyasi mmoja ulishika moto! Mwali huo ulienea kupitia unyasi mmoja na kuenenea kwa sehemu kubwa. Ulionekana wa kutisha. Kisha ukaenea!

Grace alianza kuingiwa na hofu. Upepo ulivuma na kupuliza cheche hatua chache, na moto mwingine ukaanza. Kila mtu hapo alikuwa amesahau kuhusu chakula ambacho walijianda kupika. Walikuwa kama wendawazimu wakijaribu kuzima mioto hiyo tofauti. Sasa kulikuwa na kama mioto sita tofauti. Watu walichota maji, wakarusha mchanga na kujaribu kuzima. Hatimaye kila mmoja aliweza kuzima mioto hiyo. Grace alifarijika na akawaza jinsi moto ulivyo na uhai wake wenyewe. Kwa kupepewa kidogo tu na upepo, kutoka kwa mwale ungeenea kila mahali.

Je, umewahi kusikia kuhusu 'Pembe Tatu za Moto'? Ili moto uwake unahitaji vipengele vitatu: hewa, joto na kuni. Katika hadithi yetu upepo ulileta hewa nyingi, joto likatoka kwenye moto na kuni kutokana na nyasi. Kuondoa mojawapo ya vipengele hivi vitatu moto utazima kwa sababu pembe tatu hazijakamilika

Tunaweza kufikiria Makundi ya Maisha kwa njia hii. Tuna hewa ya maombi na kujifunza neno la Mungu. Tuna joto, moto wa Roho wa Mungu pamoja nasi. Tunachohitaji ni kuni. Kweli ya Mungu inayoenezwa na kuonyeshwa kupitia mahusiano na watu ndizo kuni tunazohitaji!

Katika kitabu cha Matendo ya Mitume, tunaona kwamba kanisa la kwanza lilikua kwa kasi kutoka sehemu moja hadi nyingine. Moto wa uzima wa Mungu ulienea kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine na jinsi watu walivyosafiri, sehemu moja hadi nyingine. Kwa uwazi walinena na kudhihirisha kweli waliyoipata ndani ya Yesu. Kam asemavyo Isaya 49:6, "Zaidi ya hayo nitakutoa uwe nuru ya Wayunani (Mataifa), upate kuwa wokovuwangu hata miisho ya dunia."


### Zingatia!

Habari njema ya Yesu yapaswa kudhihirishwa na kuenezwa. Hii inamaanisha Vikundi vyetu vya Maisha havipaswi kuwa na watu wale wale kwa muda mrefu. Njia moja ya kufanya hivyo ni kuwakaribisha watu kuwa sehemu ya jamii yetu ya Vikundi vya Maisha. Tunaweza kuwakaribisha marafiki wetu na wale walio mbali nasi. Jinsi tunavyoleta kuni za mahusiano hayo na kuzijumuisha pamoja na hewa ya Mungu na joto. Tusisite kunena na kumdhihirisha Kristo katika mahusiano tuliyonayo.

### Omba:

Mungu atawandaa watu watakaozingatia mwaliko wako na kukupa maneno unayofaa kusema.

### Pembe Tatu za Moto



Bwana Mulenga\* alikuwa kwenye basi kuelekea nyumbani. Akasikia mtu akiongea na rafikiye kuhusu Mashirika ya nyumbani ya kujifunza Biblia ambayo alikuwa anasaidia watu kuyaanzisha kwenye kijiji chake.

Bwana Mulenga alivutiwa na akataka kujua zaidi. Aliinamia mbele na akujiunga na mazungumzo hayo. Akajifunza kwamba anaweza kuanzisha Kundi la Maisha katika kijiji chake.

**- Mr Mulenga,\* 16 Miles, Zambia**



Funzo hili limechochewa na "Kuwasha moto Jinsi ya Kupanda Kijijini" somo linalosaidia watu kuelewa jinsi kweli ya Mungu inafanya kazi kupitia mahusiano. Kwa maelezo zaidi:

[dignityonline.org.uk/publications](http://dignityonline.org.uk/publications)

\*Jina limebadilishwa kutunza siri za ndani